102/3
**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**
**JULAI 2013**
**MUDA: 2 ½**

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

# MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA NANDI KUSINI, MASHARIKI NA TINDIRET 2013

**CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA KIDATO CHA NNE**

**KISWAHILI**
**FASIHI**
**KARATASI YA TATU**
**MUDA: 2 ½**

**MAAGIZO**

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi Fupi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. hakikisha kwamba Maswali yote yamo.
6. kila swali linabeba alama 20.

A. **SEHEMU YA A: FASIHI (SWALI LA LAZIMA)**

1. (a) (i) Miviga ni nini? (alama 2)

   (ii) Fafanua sifa nne za miviga. (alama 8)

   (b) Taja na ueleze mbinu tano za kukusanya data ya fasihi simulizi. (alama 10)

**SEHEMU YA B: RIWAYA**

***Said A. Mohamed: Utengano***

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. "………Moyo ulimpiga wala hakuweza kujua kwa nini…akamwona jinsi alivyonawiri na kushiba nguvu, kijana mwenye sura ya kiume ya kuvutia…"

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   (b) Eleza sifa za mhusika aliyenawiri katika ndondoo. (alama 12)

   (c) Taja mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo na uzitolee mifano. (alama 4)

**au**

3. "Anwani: 'Utengano' inaafiki riwaya hii. Thibitisha. (alama 20)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

***Timothy Arege: Mstahiki Meya***

**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Hata bwana aliteswa kwa sababu ya neno. Mateso yake yalikuwa makubwa. Hayawezi kulinganishwa na tendo hili dogo."

   (a) (i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   (ii) Eleza maudhui yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo hili. (al. 4)

   (b) Fafanua matatizo sita yaliyoikabili jamii inayosawiriwa katika diwani. (alama 12)

**au**

5. "Sikio la kufa halisikii dawa." Kwa kurejelea tamthilia ya Mstahiki Meya, onyesha ukweli wa kauli hili. (alama 20)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

   Jana ilikuwepo, ikapita  
   Kwenye giza la sahau  
   Jana ilipiga kuathiri



For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Athari ijayo leo
Leo tanaijua
Na kesho tunoibashiria

Kesho ipapo na hatuijui
Kesho, itapiga au itapuliza?
Au itapita pasi na chochote
Kama moshi usio mashiko?

Kesho hatuioni
Lakini yaja…
Twaihisi
Twaihisi
**Twaimaizi**
Ipo,

**Yajongea**
Hiyo na taathira zake
Inakuja
Yasogea
Yaja mbio
Yafikia upeo unaoitwa leo
Basi kumbuka
Maisha ni ubishi, yakabili!
Maisha ni jasiri, jusurisha!
Maisha ni huzuni, yashinde!
Maisha ni msiba, uweze!

Maisha ni wajibu, tekeleza!
Maisha ni fumbo, liague!
Maisha ni tatizo, litatue!
Maisha ni ahadi, itemize!
Maisha mapambano, wana nayo!

Maisha ni zawadi, ipokee!
Maisha ni mchezo, uchezee!

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

Maisha ni nyimbo, iimbe!
Maisha ni fursa, itumie?
Maisha ni ureda, furahia!
Maisha maumbile, changamkie!
Maisha ni lengo, lifike!
Maisha ni mwendo, yaendee!
Maisha ni uzuri, ustarehee!
Maisha liwazo, yapumzikie!

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a) Lipe kichwa mwafaka shairi hili. (alama 2)

(b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (alama 6)

(c) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 4)

(d) Taja na ueleze tamathali tatu za semi alizotumia mwandishi wa shairi hili. (alama 6)

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi.

(i) Twaimaizi (alama 1)

(ii) Yajongea (alama 1)

## SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

***Ken Walibora na Said A. Mohamed: Damu Nyeusi na Hadihi nyingine.***

7. Kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi nyingine. Jadili jinsi maudhui ya ubaguzi yanavyofafanuliwa. (alama 20)